Jarida la Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania

# TARI HABARI

*Utafiti kwa Maendeleo ya Kilimo*

Toleo No. 04 | Aprili - Juni 2026 | www.tari.go.tz

## TARI NA WADAU WAADHIMISHA SIKU YA KIMATAIFA YA AFYA YA MIMEA



## ELIMU YA KILIMO SHADIDI CHA MPUNGA YAWAFIKIA WAKULIMA WILAYANI KILOSA



# MAKAMU WA RAIS AHIMIZA UTAFITI NA UBUNIFU KATIKA KUKABILIANA NA MABADILIKO YA TABIANCHI




## WAZIRI WA KILIMO AZINDUA MAADHIMISHO YA MIAKA KUMI YA TARI

# UJUMBE KUTOKA KWA MKURUGENZI MKUU

TARI
Transforming Agriculture

## BODI YA UHARIRI

**MWENYEKITI**

DKT. THOMAS BWANA
Mkurugenzi Mkuu TARI

**KATIBU**

DKT. SOPHIA KASHENGE
Mkurugenzi wa Uhaulishaji Teknolojia, Biashara na Mahusiano

**WAJUMBE**

EVELYNE MPASHA
Kaimu Meneja Menejimenti ya Maarifa na MawasilianoDKT. RAJAB KANGILE
Kaimu Meneja wa uhaulishaji wa teknolojia, uendeshaji wa biashara na ushirikiano

DKT. ABDULLAH MKIGA
Kaimu Meneja wa Kituo, TARI Kifyulilo

DKT. ANDEKILILE MWAMAHONJE
Mtafiti Mwandamizi

DEODATUS KIRIBA
Mtafiti Mwandamizi

**WAANDISHI**

MUGINI SINGIRA
Afisa Uhusiano kwa Umma

GERALD USIRI
Afisa Uhusiano kwa Umma

MARIA PAUL
Afisa Uhusiano kwa Umma

HOSEA R. BILATANGUYE
Afisa Uhusiano kwa Umma

TariTanzania | Tanzaniatari | official_taritanzania | TARI Tanzania | TARI

**NDUGU** msomaji mpendwa, Karibu tena katika toleo letu la nne la Jarida la TARI Habari Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) ina jukumu la kufanya, kusimamia, kuratibu, na kuhamasisha matumizi ya teknolojia za kisasa nchini ili kutatua changamoto za wakulima, kuongeza tija, na kuchangia maendeleo endelevu ya sekta ya kilimo na Taifa kwa ujumla.

Katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 2026, TARI ilifanya utafiti wa aina 56 za mbegu za mazao ya kimkakati, pamoja na kuboresha teknolojia za afya ya udongo na matumizi sahihi ya mbolea, ikihusisha pia zao la tumbaku ya mvuke. Aidha, taasisi ilifanya tafiti za magonjwa sugu ya mazao, ikiwemo fungashada (BBTV) kwenye migomba, blaiti ya mikorosho, pamoja na ubwiri unga na mnyauko fuzari katika zao la korosho. Sambamba na hilo, TARI iliendelea na mkakati wa kuzalisha teknolojia saba (7) za kuongeza thamani ya mazao, kusafisha na kuhifadhi aina 360 za mbegu za asili, pamoja na kukusanya vinasaba 12,968. Vilevile, taasisi iliendeleza kituo cha TARI Ifakara kuwa kituo mahiri cha utafiti wa zao la kakao na kuendelea na majaribio ya aina 82 za mbegu mpya za ngano katika mikoa ya Morogoro na Tanga.

Ili kulinda maeneo haya ya utafiti dhidi ya uvamizi, TARI imeongeza kasi ya ujenzi wa uzio katika mashamba 10 ya utafiti, huku ikihakikisha upatikanaji wa hatimiliki katika vituo 17 na mashamba ya majaribio 18. Hatua hizi zinaenda sambamba na ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaohamishwa katika kituo cha TARI Uyole. Katika kuboresha miundombinu, taasisi inaendelea na ujenzi wa kituo cha Bioscience mkoani Morogoro, benki ya mbegu katika kituo cha TARI Selian, na ofisi ya Makao Makuu iliyopo Njedengwa, Dodoma. Aidha, taasisi inaendelea na ujenzi wa ofisi katika kituo cha TARI Hombolo, pamoja na ununuzi wa vifaa vya Ofisi ya TARI Kihinga.

Katika mwaka wa fedha 2026/2027, TARI itaendelea kutekeleza shughuli mbalimbali za utafiti na ubunifu wa teknolojia za kilimo. Shughuli hizi zinajumuisha ugunduzi wa mbegu bora, uwekaji wa kanuni bora za kilimo, uboreshaji wa afya ya udongo, na udhibiti wa visumbufu vya mazao kama magonjwa na wadudu. Aidha, taasisi itajikita katika utunzaji wa nasaba za mazao pamoja na kufanya tafiti za uchumi jamii na masoko.



*DKT. THOMAS BWANA*
*MKURUGENZI MKUU - TARI*

Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya TARI ya mwaka 2026/2027 yamezingatia kwa karibu Mpango Mkakati wa TARI (2025/2026–2029/2030) na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa Serikali. Vilevile, mpango huu umezingatia Dira ya Taifa (2050), Mpango Mkuu wa Sekta ya Kilimo (Tanzania Agriculture Master Plan), pamoja na masuala mtambuka ya mapambano dhidi ya rushwa na VVU/UKIMWI.

Ili kupima ufanisi na mchango wa teknolojia zilizohaulishwa kwa wadau, TARI imepanga kufanya tathmini mbalimbali.

Tathmini hizo ni pamoja na tathmini 10 za mapokeo (adoption) ya teknolojia za kilimo, tathmini 6 za matokeo (impact) ya teknolojia hizo, pamoja na tathmini 3 za masoko na masuala ya jinsia.

TARI tuna jukumu kubwa la kuhakikisha tunaleta tija kwa wakulima wetu.

Tunakukaribisha kuendelea kuwa nasi katika mfululizo wa matoleo ya jarida letu la TARI Habari ili uweze kufahamu kwa kina namna tafiti hizi zinavyosaidia kuimarisha sekta ya kilimo nchini.






# MAKAMU WA RAIS AHIMIZA UTAFITI NA UBUNIFU KATIKA KUKABILIANA NA MABADILIKO YA TABIANCHI

**MAKAMU** wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, amezitaka taasisi za utafiti nchini kuendelea kufanya tafiti na ubunifu unaochangia uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ili kuunga mkono juhudi za Serikali katika kufikia maendeleo endelevu.

Mhe.Dkt. Nchimbi alitoa wito huo Juni 5, 2026, wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani ambayo kitaifa yalifanyika katika Viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dodoma, akimwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Katika hotuba yake, Mhe. Dkt. Nchimbi alisisitiza umuhimu taasisi zinazofanya utafiti nchini kubuni mbinu mbadala zitakazosaidia utunzaji wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni pamoja na kuongeza matumizi ya nishati safi ya kupikia, kuimarisha usimamizi wa taka kupitia mifumo ya uchumi mviringo.

Maadhimisho hayo yalitanguliwa na wiki ya maonesho iliyoanza Juni 1, 2026, chini ya kaulimbiu isemayo "Dira 2050: Tuwajibike Kukijanisha Tanzania," ambapo taasisi mbalimbali za Serikali na sekta binafsi zilipata fursa ya kuonesha mchango wao katika utunzaji wa mazingira na maendeleo endelevu.

Katika hatua nyingine, Mhe. Dkt. Nchimbi alitembelea mabanda mbalimbali ya maonesho yaliyokuwa katika viwanja hivyo ambapo katika banda la Wizara ya Kilimo, alipokelewa na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo anayesimamia Umwagiliaji na Zana za Kilimo, Mhe. Athumani Kilundumya na kumtembeza katika mabanda ya Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Kilimo.

Akiwa katika banda la TARI, Mkurugenzi Mkuu wa TARI Dkt. Thomas Bwana alimueleza Makamu wa Rais kuhusu teknolojia mbalimbali za kilimo himilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi zinazotafitiwa na kuendelezwa na TARI kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mazao, kuhifadhi mazingira na kuimarisha usalama wa chakula nchini.

Dkt. Bwana amezitaja teknolojia hizo kuwa ni pamoja na matumizi ya mbegu bora zinazostahimili ukame, magonjwa na wadudu pamoja na mbinu endelevu za usimamizi wa udongo na maji

TARI inaendelea kuunga mkono juhudi za Serikali kupitia tafiti na ubunifu wa teknolojia za kilimo endelevu zinazochangia uhifadhi wa mazingira, kuongeza tija kwa wakulima na kuimarisha ustahimilivu wa sekta ya kilimo dhidi ya athari za mabadiliko ya tabianchi.



# BAJETI YA WIZARA YA KILIMO YAPITISHWA, MIUNDOMBINU YA UTAFITI KUIMARISHWA

**BUNGE** la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limepitisha Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2026/2027, huku Serikali ikiweka mkazo katika kuimarisha utafiti wa kilimo, kuongeza uzalishaji na kuendeleza miundombinu ya kisasa ya sekta hiyo.

Akiwasilisha bajeti hiyo bungeni, Waziri wa Kilimo, Mhe. Daniel Godfrey Chongolo (Mb), alisema Wizara ya Kilimo imepanga kutumia jumla ya shilingi trilioni 1.19, ambapo kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 961.69 zimetengwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo na shilingi bilioni 231.28 zimetengwa kwaajili ya matumizi ya kawaida.

Mpango wa mwaka ujao umejikita katika maono ya kuifikisha Tanzania kwenye hadhi ya uchumi wa kipato cha kati cha juu ifikapo mwaka 2050 kupitia vipaumbele sita vya kimkakati.

Kwa mujibu wa Mhe. Chongolo, vipaumbele hivyo ni kuongeza tija na uzalishaji wa mazao, kuzalisha ajira zenye staha kwa vijana na wanawake, kuimarisha usalama wa chakula na lishe bora, pamoja na kupanua wigo wa upatikanaji wa mitaji, masoko na fursa za mauzo ya mazao katika masoko ya nje.

Katika eneo la utafiti wa kilimo, Mhe. Chongolo, alisema Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imeendelea kuimarisha mchango wake kwa kufanya utafiti wa aina 30 za mbegu za mazao ya kimkakati.

Aidha, TARI imefanikiwa kuhifadhi aina 54 za mbegu za asili zenye uwezo mkubwa wa kustahimili ukame na magonjwa, hatua inayolenga kusaidia juhudi za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kuimarisha usalama wa chakula nchini.



Waziri Chongolo pia alieleza kuwa Serikali inaendelea kuwekeza katika miundombinu ya kisasa ya utafiti, ambapo ujenzi wa Maabara ya Kudhibiti Visumbufu vya Mimea umefikia asilimia 60, huku ujenzi wa Maabara ya Teknolojia ya Chupa (Tissue Culture) ukifikia wastani wa asilimia 30.

Kwa upande wa mchango wa sekta ya kilimo katika uchumi wa Taifa, Mhe. Chongolo, alisema sekta hii iliendelea kuwa uti wa mgongo wa uchumi mwaka 2025 kwa kukua kwa asilimia 4.0 na kuchangia asilimia 24.6 katika pato la taifa (GDP).

Wakati huo huo, Wizara imeweka lengo la kuongeza uzalishaji wa mazao ya kimkakati hadi kufikia tani 1,599,945.66 katika msimu wa 2025/2026, sawa na ongezeko la asilimia 10 ikilinganishwa na tani 1,451,694.11 zilizozalishwa katika msimu wa 2024/2025.

Hatua hiyo inatarajiwa kuongeza tija, kuimarisha usalama wa chakula na kuchochea ukuaji wa uchumi kupitia sekta ya kilimo ambayo inaendelea kuwa mhimili muhimu wa maendeleo ya Tanzania.




# WAZIRI WA KILIMO AZINDUA MAADHIMISHO YA MIAKA KUMI YA TARI

**WAZIRI** wa Kilimo, Mhe. Daniel Chongolo (Mb) amezindua rasmi maadhimisho ya miaka kumi ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) na kuagiza sherehe za maadhimisho hayo zifanyike Agosti, 2026 katika kipindi cha maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Nanenane ili kutoa fursa kwa wadau wengi zaidi kushiriki.

Mhe. Chongolo ametoa agizo hilo Aprili 23, 2026 katika ukumbi wa Wizara ya Kilimo (Kilimo IV) na kueleza ushiriki wake katika maadhimisho hayo huku akipongeza mchango mkubwa wa TARI katika kuleta mageuzi ya sekta ya kilimo nchini kupitia utafiti ndani ya kipindi cha miaka kumi.

Katika pongezi hizo, Mhe. Chongolo alifananisha mchango huo wa TARI na uimara wa nyumba ambao hutegemea msingi na kubainisha kuwa TARI ni msingi muhimu wa maendeleo ya sekta ya kilimo nchini.

Katika hafla ya uzinduzi huo, Mhe. Chongolo pia alizindua jezi maalum ya TARI itakayotumika katika TARI Marathon ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 10 ya TARI. Pia alikabidhi jumla ya pikipiki 71 kwa taasisi hiyo ili kuongeza ufanisi wa kazi kwa watafiti katika vituo mbalimbali vya utafiti na mashamba ya majaribio kote nchini ili kuharakisha utoaji wa matokeo ya tafiti kwa wakulima na wadau wengine katika mnyororo wa kilimo.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa TARI Dkt. Thomas Bwana alimshukuru Mhe. Chongolo kwa kukubali kujumuika na TARI katika hafla ya uzinduzi wa miaka kumi ya taasisi hiyo.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwemo Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Silinde (Mb), Naibu Katibu Mkuu anayesimamia Umwagiliaji na Zana za Kilimo, Mheshimiwa Mhandisi Athumani Kilundumya, Menejimenti ya TARI na watumishi kutoka TARI Makao Makuu, TARI Hombolo na TARI Makutopora.

## DIRA & DHIMA

**DIRA:** Kuwa Kituo cha Kimataifa cha ubora katika utafiti wa kilimo kwa maendeleo endelevu.
**DHIMA:** Kuendeleza, kusambaza na kutoa mwongozo wa kisera kuhusu teknolojia zinazofaa za kilimo ili kuboresha maisha ya wananchi.



# TARI: ILIPOTOKA, ILIPO NA INAPOELEKEA

## Safari kutoka DRD hadi TARI

**TAASISI** ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) ni taasisi ya kitaifa inayosimamia utafiti wa kilimo nchini Tanzania. Kuanzishwa kwake ni matokeo ya mageuzi ya muda mrefu yaliyolenga kuimarisha utafiti wa kilimo na kuhakikisha matokeo ya tafiti yanawafikia wakulima kwa ufanisi zaidi.

Baada ya Uhuru mwaka 1961, shughuli za utafiti wa kilimo zilisimamiwa na Idara ya Utafiti na Maendeleo (Department of Research and Development – DRD) chini ya Wizara ya Kilimo. Kwa miongo kadhaa, DRD ilisimamia vituo mbalimbali vya utafiti nchini na kuzalisha teknolojia nyingi zilizosaidia kuongeza uzalishaji wa mazao, mifugo na maliasili za kilimo.

Kadiri mahitaji ya sekta ya kilimo yalivyoongezeka na changamoto mpya kama mabadiliko ya tabianchi, ongezeko la watu na ushindani wa masoko zilivyojitokeza, Serikali iliona umuhimu wa kuwa na taasisi maalumu yenye mamlaka na uwezo mpana zaidi wa kusimamia utafiti wa kilimo. Mwaka 2016, Serikali ilianzisha TARI kupitia Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania Na. 10 ya mwaka 2016, ikichukua rasmi majukumu yaliyokuwa yakitekelezwa na DRD. Hatua hii ililenga kuongeza ufanisi, ubunifu na ushirikiano katika kufanya tafiti zenye kuleta tija kwa wakulima na maendeleo ya taifa.

Wakati Serikali ilipoanzisha TARI kupitia Sheria Na. 10 ya mwaka 2016, haikuanza kutoka sifuri, badala yake, ilifanya mageuzi ya mfumo wa usimamizi wa utafiti wa kilimo kwa kuhamisha majukumu ya utafiti wa kilimo kutoka DRD kwenda TARI, kuhamisha watumishi waliokuwa wakitekeleza shughuli za utafiti chini ya DRD kwenda TARI kwa kuzingatia taratibu za utumishi wa umma, kurithisha vituo vya utafiti, miundombinu, mashamba ya majaribio, maabara, vifaa vya utafiti na miradi iliyokuwa chini ya DRD na kuendeleza programu za utafiti na ushirikiano wa kitaifa na kimataifa uliokuwepo kabla ya kuanzishwa kwa TARI.

TARI pia ilirithi aina nyingi za mbegu na teknolojia zilizokuwa zimezalishwa na DRD, mtandao wa vituo vya utafiti vilivyoenea nchini pamoja na mahusiano na wakulima, taasisi za elimu ya juu, sekta binafsi na washirika wa maendeleo.

TARI ndiyo taasisi kuu ya utafiti wa kilimo nchini Tanzania. Ina makao makuu yake Mkoani Dodoma na inaratibu mtandao wa vituo 20 vya utafiti na vituo vidogo 25 vya majaribio vilivyopo katika Kanda mbalimbali za nchi, kila kimoja kikijikita katika mazao na mifumo ya kilimo inayofaa mazingira ya Kanda husika.

Katika kipindi cha muongo wa kwanza, TARI imefanikiwa kuendeleza na kuzalisha mbegu bora za mazao mbalimbali. kubuni teknolojia zinazoongeza uzalishaji na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. kuimarisha afya ya udongo na usimamizi wa rasilimali za kilimo pamoja na kukuza matumizi ya teknolojia za kisasa na kilimo cha kidijitali.

Aidha, TARI pia imefanikiwa kushirikiana na vyuo vikuu, sekta binafsi, mashirika ya kimataifa na wakulima katika kufanya tafiti shirikishi, kuchangia kuongezeka kwa uzalishaji, usalama wa chakula na kipato cha wakulima kupitia ubunifu wa kisayansi na kuendelea kuhamasisha matumizi ya matokeo ya tafiti kwa kuhakikisha teknolojia zinawafikia watumiaji kupitia maonesho, mashamba darasa, mafunzo na ushirikiano na huduma za ugani.

TARI inalenga kuwa taasisi ya kimataifa yenye ubora katika utafiti wa kilimo unaochochea maendeleo endelevu ya Tanzania. TARI ya kesho inalenga Katika miaka ijayo, TARI inalenga kuongeza matumizi ya akili unde (AI), teknolojia za kidijitali na uchambuzi wa data katika utafiti wa kilimo, kubuni mazao yenye uwezo mkubwa wa kustahimili ukame, magonjwa na athari za mabadiliko ya tabianchi kuongeza thamani ya mazao kupitia teknolojia za baada ya kuvuna.

Na kupanua ushirikiano na sekta binafsi ili tafiti zibadilike kuwa bidhaa na huduma zinazowanufaisha wakulima.

Aidha, TARI pia ina mkakati wa kukuza kilimo chenye tija, ushindani na rafiki kwa mazingira ikiwa ni pamoja na kusaidia utekelezaji wa sera za taifa zinazolenga usalama wa chakula, maendeleo ya viwanda vya kilimo na uchumi wa Taifa.

Leo, TARI inaendelea kuwa nguzo muhimu ya mageuzi ya sekta ya kilimo, ikitengeneza teknolojia zinazoongeza uzalishaji, zinajenga ustahimilivu dhidi ya changamoto za tabianchi, na zinaweka msingi wa Tanzania yenye kilimo cha kisasa, chenye tija na ushindani katika soko la kikanda na kimataifa. Hongera Timu nzima ya Watumishi wa TARI, Wakulima na Wadau washirika wa maendeleo ya Kilimo katika Maadhimisho ya miaka 10 yenye mafanikio katika sekta ya kilimo.

# VITUO VYA UTAFITI TARI






# TARI NA WADAU WAADHIMISHA SIKU YA KIMATAIFA YA AFYA YA MIMEA

**TAASISI** ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa sekta ya kilimo, imeadhimisha Siku ya Kimataifa ya Afya ya Mimea katika viwanja vya John Samuel Malecela, Nzuguni jijini Dodoma, Mei 12, 2026.

Maadhimisho hayo yameratibiwa na Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) yenye kaulimbiu "Ulinzi wa Bayoanuai ya Mimea kwa Usalama wa Chakula na Lishe". Maadhimisho hayo hufanyika kila mwaka tarehe 12 Mei kwa lengo la kuongeza uelewa kuhusu umuhimu wa afya ya mimea katika kuhakikisha usalama wa chakula na lishe, kukuza biashara na maendeleo endelevu duniani.

Maadhimisho hayo yalianza kwa maonesho tarehe 10 Mei na kuhitimishwa tarehe 12 Mei 2026, yakihusisha TARI na wadau mbalimbali wa sekta ya kilimo.

Akihutubia wananchi wakati wa maadhimisho hayo, Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. David Silinde (Mb) ambaye amemwakilishe Waziri wa Kilimo Mhe. Daniel Chongolo (Mb), amesema mimea ni msingi wa maisha duniani kwa kuwa ndiyo chanzo cha chakula, dawa pamoja na malighafi za viwandani na kuongeza kuwa Wizara ya Kilimo itaendelea kuimarisha utendaji kazi wa TPHPA ili kuhakikisha huduma bora za usimamizi wa afya ya mimea zinaendelea kutolewa nchini kwa lengo la kukuza sekta ya kilimo na kufikia Agenda 10/30 pamoja na Dira2050.

Aidha, Mhe. Silinde amempongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa juhudi zake za kuimarisha huduma za kidijitali nchini, hatua ambayo imeendelea kuleta manufaa makubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Silinde alisisitiza umuhimu wa kuongeza juhudi katika kulinda bayoanuai ya mimea kwa ajili ya kuimarisha usalama wa chakula na lishe.

Aidha, Mheshimiwa Silinde alitembelea mabanda mbalimbali ya maonyesho ambapo katika banda la TARI, Mkurugenzi wa Utafiti na Ubunifu Dkt. Deusdedith Mbanzibwa alimueleza Mhe.Silinde kuhusu mchango wa TARI katika kuimarisha afya ya mimea. Mhe. Naibu alielezwa kuhusu teknolojia zinazolinda afya ya mimea ambazo ni kinzani kwa wadudu na magonjwa . Teknolojia hizo ni Maharage aina ya JESCA, LYAMUNGO 85, TARIBEAN 6,7 na SELIAN 13. Teknolojia nyingine ni Mbaazi aina ya Mali, SOYA aina ya UYOLE.Karanga aina ya TARIKA 1 na TARIKA 2, Ufuta aina ya LINDI 2002, Zabibu ya kukaushwa na Mvinyo.





# KIJUE KITUO CHA TARI MIKOCHENI

**TARI** Mikocheni ni mojawapo ya vituo 20 vya utafiti vilivyoko chini ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), pia ni kati ya vituo vituo vitatu (3) vinavyounda kanda ya mashariki.

Kituo cha TARI Mikocheni kilianzishwa mwaka 1979 kikiwa na malengo makuu mawili ambayo ni kufanya na kuendeleza utafiti kwa maendeleo ya sekta ndogo ya minazi nchini na lengo linguine ni kuratibu, kufanya na kuendeleza utafiti na matumizi ya Biloteknolojia kwenye sekta ya kilimo kwa manufaa ya uchumi jamii nchini.

Kituo hiki kipo mkoani Dar es salaam na kinaundwa na vituo vidogo viwili(2) ambavyo ni Chambezi kilichopo kilometa 55 kaskazini mwa Dar es Salaam, Wilaya ya Bagamoyo na Mkuranga kilichopo kilometa 50 kusini mwa Dar es Salaam, Wilaya ya Mkuranga. Vituo hivi vidogo ni kwa ajili ya majaribio ya utafiti shambani(Field trials).

**HUDUMA ZITOLEWAZO NA KITUO**

i.Ushauri wa kanuni bora za kilimo cha minazi kwa wadau mbalimbali wa kilimo.

Mtafiti akitoa elimu ya kanuni bora za kilimo cha minazi kwa mkulima

ii.Usambazaji na ugawaji wa Miche bora ya minazi mirefu aina ya asili (East African Tall) kwa wakulima na halmashauri zinazolima zao la minazi.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga Mhe. Balozi Dkt. Batilda Burian akikabidhi miche




ya minazi kutoka TARI Mikocheni kwa wakulima wa kijiji cha Songa Batini wilaya ya Muheza mkoani Tanga.

iii.Kilimo Mseto cha minazi na mazao mengine mfano; matunda mbalimbali, mahindi, mihogo, maharage n.k.

iv. Uchunguzi wa kimaabara wa magojwa yanayosumbua mimea.

v.Uzalishaji wa mimea kwa njia ya chupa (Tissue culture) mfano; mananasi,ndizi, mihogo,viazi vitamu,n.k.



vi.Usindikaji wa mazao yatokanayo na minazi mfano; "Mafuta Mwali ya Nazi".

Hatua za usindikaji wa mafuta mwali ya nazi

vii.Teknolojia za udhibiti wa visumbufu vya minazi - udhibiti wa mdudu chonga (Rhinocerous beetle) kwa kutumia ndoano, udhibiti wa utitiri wa minazi (coconut mites) na udhibiti wa mbu wa minazi (coconut bug).

Mtafiti akielezea namna ya kumtoa mdudu chonga kwenye mnazi kwa kutumia ndoano

viii. Mafunzo kwa wadau mbalimbali wa kilimo mfano wakulima, wanafunzi n.k.

TARI Mikocheni imejikita katika utafiti na usambazaji wa teknolojia mbalimbali zinazogunduliwa na watafiti wa kilimo; mfano matumizi bora ya mbinu za kilimo zikiwemo mbegu bora za minazi (EAST AFRICAN TALL) zenye kustahimili ukame na zinazo kinzana na magonjwa na wadudu, kilimo mseto, matumizi bora ya mbolea na utunzaji wa mashamba kulingana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Kituo kimejizatiti kupeleka elimu na maarifa kwa wakulima kuhusu kilimo cha minazi ili kuwajengea uwezo wakulima kwa njia ya mafunzo, mashamba darasa, semina na mikutano. Kuhamasisha na kutangaza kilimo cha zao la minazi na mazao mengine katika mnyororo wa thamani katika mfumo mzima wa uzalishaji, usindikaji na uuzaji wake.

Kituo kinaendelea kufanya utafiti unaolenga kutatua changamoto zinazowakabili wakulima wa minazi nchini.



*Mtafiti akitoa elimu ya kanuni bora za kilimo cha minazi kwa mkulima*

**HUDUMA ZITOLEWAZO NA KITUO**

i.Ushauri wa kanuni bora za kilimo cha minazi kwa wadau mbalimbali wa kilimo.

ii.Usambazaji na ugawaji wa Miche bora ya minazi mirefu aina ya asili (East African Tall) kwa wakulima na halmashauri zinazolima zao la minazi.

iii.Kilimo Mseto cha minazi na mazao mengine mfano; matunda mbalimbali, mahindi, mihogo, maharage n.k.

v.Uzalishaji wa mimea kwa njia ya chupa (Tissue culture) mfano; mananasi,ndizi, mihogo,viazi vitamu,n.k.

vi.Usindikaji wa mazao yatokanayo na minazi mfano; "Mafuta Mwali ya Nazi".

vii. eknolojia za udhibiti wa visumbufu vya minazi - udhibiti wa mdudu chonga (Rhinocerous beetle) kwa kutumia ndoano, udhibiti wa utitiri wa minazi (coconut mites) na udhibiti wa mbu wa minazi (coconut bug).

viii.Mafunzo kwa wadau mbalimbali wa kilimo mfano wakulima, wanafunzi n.k.

TARI Mikocheni imejikita katika utafiti na usambazaji wa teknolojia mbalimbali zinazogunduliwa na watafiti wa kilimo; mfano matumizi bora ya mbinu za kilimo zikiwemo mbegu bora za minazi (EAST AFRICAN TALL) zenye kustahimili ukame na zinazo kinzana na magonjwa na wadudu, kilimo mseto, matumizi bora ya mbolea na utunzaji wa mashamba kulingana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Kituo kimejizatiti kupeleka elimu na maarifa kwa wakulima kuhusu kilimo cha minazi ili kuwajengea uwezo wakulima kwa njia ya mafunzo, mashamba darasa, semina na mikutano. Kuhamasisha na kutangaza kilimo cha zao la minazi na mazao mengine katika mnyororo wa thamani katika mfumo mzima wa uzalishaji, usindikaji na uuzaji wake.

Kituo kinaendelea kufanya utafiti unaolenga kutatua changamoto zinazowakabili wakulima wa minazi nchini.





*Mkuu wa Mkoa wa Tanga Mhe. Balozi Dkt. Batilda Burian akikabidhi miche ya minazi kutoka TARI Mikocheni kwa wakulima wa kijiji cha Songa Batini wilaya ya Muheza mkoani Tanga.*









*Mtafiti akielezea namna ya kumtoa mdudu chonga kwenye mnazi kwa kutumia ndoano*







*Hatua za usindikaji wa mafuta mwali ya nazi*



# ELIMU YA KILIMO SHADIDI CHA MPUNGA YAWAFIKIA WAKULIMA WILAYANI KILOSA

**WAKULIMA** wa Mpunga wameshauriwa kutumia kanuni bora za kilimo shadidi cha Mpunga kinachohimiza matumizi ya mbegu kidogo, maji kidogo lakini mavuno mengi ili kuongeza uzalishaji tija katika zao hilo.

Wito huo umetolewa Mei 22, 2026 na Mtafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Dkt. Atugonza Bilaro katika siku ya mkulima wa Mpunga iliyofanyika katika skimu ya Ilonga, Wilaya ya Kilosa, Mkoa wa Morogoro kwa lengo la kuhamasisha kanuni bora za kilimo shadidi cha Mpunga.

Kwa upande wake, Afisa Tarafa ya Kimamba, Bi. Sabina Lucas akimwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Kilosa ameipongeza TARI baada ya kupewa taarifa ya kufikisha elimu ya kilimo shadidi cha Mpunga kwa wakulima zaidi ya elfu nne katika maeneo mbalimbali yanayolima Mpunga nchini.



Akielezea faida za kilimo shadidi cha mpunga Mkulima wa Mpunga skimu ya Ilonga Bwana Alex Mwinuka ametaja baadhi ya faida hizo kuwa ni pamoja na matumizi ya mbegu kidogo ambapo zamani anasema alikuwa akitumia zaidi ya kilo kumi kupanda ekari moja lakini baada ya kupata mafunzo kutoka TARI kupitia kitalu mkeka anapanda ekari moja kwa kilo mbili.

Naye Mkulima Godfrey Paschal anasema katika kilimo cha mazoea alikuwa akivuna wastani wa gunia nane hadi kumi kwa ekari lakini katika kilimo shadidi anavuna wastani wa gunia 30-35 kwa ekari.



# MAAFISA UGANI WAAGIZWA KUHAULISHA TEKNOLOJIA YA KILIMO SHADIDI

**MAAFISA** ugani Wilaya ya Bunda, Mkoa wa Mara wameelekezwa kuhaulisha teknolojia ya kilimo shadidi cha Mpunga kwa wakulima wa zao hilo katika maeneo mbalimbali ambayo zao la mpunga linalimwa.

Agizo hilo limetolewa Mei 26, 2026 na Mkuu wa Wilaya ya Bunda Mheshimiwa Aswege Kaminyoge katika siku ya Mkulima wa zao la Mpunga iliyofanyika katika skimu ya Mariwanda, Wilaya ya Bunda, Mkoa wa Mara, ikiwa na lengo la kutoa elimu ya kilimo shadidi cha Mpunga kinachohimiza matumizi ya Mbegu kidogo, maji kidogo lakini mavuno mengi.

Akizungumza katika shamba la mmoja wa wakulima wanaolima kwa kufuata kanuni za kilimo shadidi, Mhe. Kaminyoge ameipongeza Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kwa kupeleka teknolojia hiyo na kusema sasa ni jukumu la maafisa ugani kuhakikisha teknolojia hiyo inawafikia wakulima wengi zaidi ili kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja, Halmashauri na taifa kwa ujumla.



Akieleza kuhusu kilimo hicho, Mkulima wa Mpunga skimu ya Mariwanda Bi Dorica Biseko amesema tangu aanze kulima shadidi mavuno yameongezeka kutoka wastani wa gunia kumi na tano kwa ekari kufikia wastani wa gunia thelathini na tano kwa ekari.

Kwa upande wake Mtafiti kutoka TARI, Dkt. Atugonza Bilaro amesema lengo la kuhimiza kilimo hicho ni kutatua changamoto za matumizi ya gharama kubwa katika uzalishaji wa zao la Mpunga na kumuongezea Mkulima tija katika eneo dogo.

Dkt. Bilaro ambaye pia ni Mratibu wa Mradi wa kilimo shadidi unaotekelezwa katika Halmashauri za Bunda, Chalinze, Iringa Vijijini, Kilombero, Mbarali na Kilosa amesema wakati mradi unaanzishwa mwaka 2022 ulikuwa na lengo la kuwafikia wakulima wa Mpunga 2000 lakini hadi sasa wamefanikiwa kufikia zaidi ya Wakulima elfu sita katika maeneo mbalimbali.



# WAKULIMA WILAYANI MKINGA WANUFAIKA NA MICHE YA MINAZI KUTOKA TARI

**TAASISI** ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), kupitia Kituo cha TARI Mikocheni, imeshiriki uzinduzi wa ugawaji wa miche ya minazi uliofanyika Kijiji cha Bwiti, Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga mkoani Tanga, kama sehemu ya ushirikiano na Halmashauri hiyo katika kuimarisha uzalishaji wa zao la minazi.

Uzinduzi huo ulihudhuriwa na Mkuu wa Wilaya ya Mkinga, Mhe. Gilbert Kalima, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Tanga, pamoja na viongozi mbalimbali wa serikali, watendaji wa wilaya, maafisa kilimo na wakulima. Kwa upande wa TARI, Mkurugenzi Mkuu aliwakilishwa na Dkt. Fred Tairo, akiwa pamoja na Meneja wa Kituo cha TARI Mikocheni, Bi. Evangelista Chiunga.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mhe. Kalima alisisitiza umuhimu wa kuimarisha uzalishaji wa minazi kupitia matumizi ya miche bora na teknolojia za kisasa ili kuongeza tija na kipato cha wakulima. Kaulimbiu ya tukio hilo ilikuwa "Uzinduzi wa Kugawa Miche ya Minazi kwa Maendeleo yetu, kwa Kesho yetu."

Jumla ya wananchi 412 walishiriki katika zoezi la ugawaji huo ambapo miche 3,700 iligawiwa kwa wakulima.

Mhe. Kalima alibainisha kuwa uzalishaji wa minazi mkoani Tanga umepungua kutokana na kuzeeka kwa mashamba ya zamani ya zao hilo hali inayochangia kupanda kwa bei ya nazi kutoka shilingi 500 hadi kufikia shilingi 1,000 kwa nazi moja.

Kupitia ushirikiano huu, TARI ilitoa mbegu 6,000 za minazi na Halmashauri ikaweka eneo na kusimamia kitalu hadi hatua ya ugawaji wa miche hiyo ikiwa ni sehemu ya juhudi za TARI kuendelea kusambaza teknolojia za kilimo cha minazi nchini ili kuongeza uzalishaji na kipato cha Wakulima.










# WAKULIMA KIGOMA WATEMBELEA TARI UYOLE KWA MAFUNZO YA UZALISHAJI WA MBEGU ZA MAHARAGE NA ALIZETI

**WAKULIMA** 13 kutoka Mkoa wa Kigoma, kupitia Mradi wa Kilimo Tija Kigoma (KiTiKi) unaofadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) na kutekelezwa na World Vision Tanzania kwa kushirikiana na Good Neighbors Tanzania, wamenufaika na mafunzo ya uzalishaji wa mbegu bora za maharage na alizeti yaliyotolewa na Kituo cha TARI Uyole.

Wakulima hao (wanaume 11 na wanawake 2) walifanya ziara ya mafunzo ya siku tatu ambapo walipokelewa na Mkurugenzi wa TARI Uyole, Dkt. Emmanuel Mrema pamoja na Mratibu wa Uhaulishaji wa Teknolojia na Mahusiano, Dkt. Owekisha Kwigizile, ambaye aliwaongoza katika kipindi chote cha mafunzo.

Katika mafunzo hayo, wakulima walipata elimu ya nadharia katika ukumbi wa "Nane Nane Farm" na mafunzo ya vitendo katika mashamba ya uzalishaji mbegu ya TARI Uyole. Mafunzo yalitolewa na watafiti wa TARI Uyole akiwemo Gregory Bundala (maharage), Boniface Mavukilo na Beatha Keffa (alizeti) waliowawezesha wakulima kuelewa mbinu bora za uzalishaji wa mbegu.

Aidha, wakulima hao walifanya ziara katika taasisi na viwanda mbalimbali ikiwemo Kiwanda cha kuchakata mazao cha Raphael Group, Kampuni ya AG Products, pamoja na Kikundi cha wakulima cha Zinduka kilichopo Mshewe, Wilaya ya Mbeya Vijijini. Ziara hizo ziliwapa uelewa wa mnyororo mzima wa thamani kuanzia uzalishaji hadi masoko ya mazao na mbegu.

Katika hatua nyingine, wakulima hao walitembelea pia Kituo cha Utabiri wa Hali ya Hewa cha TARI Uyole, ambapo walielimishwa kuhusu umuhimu wa kutumia taarifa za hali ya hewa katika kupanga shughuli za kilimo cha mbegu na uzalishaji kwa ujumla.

Kwa upande wake, Mratibu wa Mradi wa KiTiKi kutoka World Vision Tanzania kwa Wilaya za Kibondo na Kakonko, Samson S. Katabila, aliishukuru TARI kwa kuwapatia mafunzo yenye kugusa mnyororo mzima wa thamani ya mazao hayo.

Wakulima hao pia wamekubaliana kushirikiana na TARI katika uzalishaji wa mbegu za maharage na alizeti zilizothibitishwa ubora (QDS) kwa ajili ya msimu ujao.








# WAKULIMA HOMBOLO WAELIMISHWA JUU YA KUKABILIANA NA MABADILIKO YA TABIANCHI

**KITUO** cha TARI Hombolo kinachojihusisha na utafiti wa mazao ya nyanda kame na teknolojia zinazostahimili mabadiliko ya tabianchi, kimeratibu na kuadhimisha Siku ya Mkulima iliyofanyika Mei 5, 2026 katika Kata ya Hombolo, jijini Dodoma juu ya mabadiliko ya tabianchi.

Maadhimisho hayo ambayo yamefadhiliwa na mradi wa KAFACI (Korea-Africa Food and Agriculture Cooperation Initiative), unaolenga kuendeleza na kusambaza teknolojia himilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi kwa wakulima nchini Tanzania yalifunguliwa na Meneja wa Kituo cha TARI Hombolo, Dkt. Emmanuel Chilagane, ambaye alisema lengo la tukio hilo ni kuwakutanisha wakulima na watafiti ili kujadili changamoto mbalimbali za kilimo na kutafuta suluhisho kupitia teknolojia bunifu na endelevu.

Dkt. Chilagane alieleza kuwa kituo hicho kimepanua wigo wa tafiti kwa mazao mbalimbali ikiwemo ufuta, mbaazi, tende, mahindi pamoja na miche ya matunda huku akisisitiza umuhimu wa wakulima kushirikiana na TARI ili kuongeza tija ya uzalishaji na kuinua kipato chao.

Kwa upande wake, mkulima na Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Hombolo Bwawani, Bw. Noah Madeje, aliishukuru TARI kwa kutoa elimu kuhusu mbegu bora, matumizi sahihi ya udongo na umuhimu wa taarifa za hali ya hewa akisema elimu hiyo itasaidia kuongeza uzalishaji na kipato cha wakulima, na kuahidi kuitekeleza kwa vitendo elimu waliyoipata ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Akifunga maadhimisho hayo kwa niaba ya Mkurugenzi wa Uhaulishaji Teknolojia na Mahusiano wa TARI, mtafiti kutoka TARI Makao Makuu Bi. Stela Hangambage, alipongeza Kituo cha TARI Hombolo kwa kuandaa na kuadhimisha siku ya Mkulima na kuwataka wakulima kuendeleza ushirikiano na TARI ili kupata taarifa sahihi na teknolojia zitakazosaidia kuboresha kilimo chao na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.









*Mabaki ya mazao shambani husaidia kuhifadhi unyevu wa udongo, kupunguza mmomonyoko wa ardhi na kuboresha rutuba ya udongo.*

# KILIMO HIFADHI: SULUHISHO LA UHIFADHI WA MAZINGIRA NA UZALISHAJI ENDELEVU WA MAZAO

**KILIMO** hifadhi ni mfumo wa uzalishaji wa mazao unaozingatia matumizi bora ya udongo, maji na mabaki ya mazao kwa lengo la kudumisha afya ya udongo na mazingira kwa ujumla. Mfumo huu unajengwa katika kanuni kuu tatu ambazo ni kupunguza au kutolima kabisa udongo mara kwa mara, kufunika uso wa udongo kwa mabaki ya mazao au mimea funika, na kufanya mzunguko wa mazao katika msimu mmoja hadi mwingine.

Katika kipindi hiki ambacho dunia inakabiliwa na changamoto za mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa ardhi na kupungua kwa rutuba ya udongo, matumizi ya teknolojia za kilimo zinazohifadhi mazingira yamekuwa muhimu zaidi kuliko wakati mwingine wowote. Miongoni mwa teknolojia zinazopendekezwa na wataalamu wa kilimo ni kilimo hifadhi, ambacho kimeendelea kusaidia wakulima kuongeza uzalishaji huku kikilinda rasilimali za asili.

Teknolojia hii hutumika katika uzalishaji wa mazao mbalimbali yakiwemo mahindi, mtama, uwele, maharage, choroko, kunde, njugu mawe, soya na alizeti. Mazao ya jamii ya mikunde yanapendekezwa zaidi katika mzunguko wa mazao kutokana na uwezo wake wa kuongeza nitrojeni kwenye udongo na kuboresha rutuba kwa njia ya asili.

Nchini Tanzania, kilimo hifadhi kinatumika katika maeneo mbalimbali hususan yale yanayokabiliwa na changamoto za ukame na mmomonyoko wa udongo. Baadhi ya maeneo hayo ni pamoja na mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga na Manyara. Mikoa mingine ni Katavi, Rukwa, Mbeya, Songwe, Iringa na Njombe ambapo wakulima wamenufaika na teknolojia hii katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

## LUGHA ZA KILIMO

### Maana ya neno "KIHISI" katika kilimo

Katika kilimo, kihisi (sensor) ni kifaa kinachotumika kupima au kugundua hali mbalimbali za shamba ili kumsaidia mkulima kufanya maamuzi sahihi kwa kutumia taarifa halisi kutoka shambani. Kuna Kihisi cha unyevu wa udongo, kihisi cha joto, kihisi cha mvua, kihisi cha virutubisho katika udongo, kihisi cha upepo, n.k.



***Mzunguko wa mazao husaidia kuboresha rutuba ya udongo, kupunguza magonjwa na wadudu waharibifu wa mazao pamoja na kuongeza uzalishaji.***

Mbali na kuongeza uzalishaji, kilimo hifadhi kina mchango mkubwa katika utunzaji wa mazingira. Kwanza, hupunguza mmomonyoko wa udongo kwa kuwa mabaki ya mazao yanayofunika ardhi hulinda udongo dhidi ya nguvu ya matone ya mvua na upepo. Hali hii husaidia kuhifadhi tabaka la juu la udongo ambalo lina rutuba nyingi zinazohitajika kwa ukuaji wa mazao.

Pili, kilimo hifadhi husaidia kuhifadhi unyevu wa udongo kwa kupunguza kasi ya uvukizaji wa maji. Hii huongeza uwezo wa mazao kustahimili vipindi vya ukame na kutumia vizuri maji yanayopatikana kwenye udongo.

Aidha mabaki ya mazao yanapooza huongeza kiasi cha mboji na virutubisho kwenye udongo, jambo linaloboresha rutuba na muundo wa udongo kwa muda mrefu. Udongo wenye afya nzuri huwa na uwezo mkubwa wa kuhifadhi maji na virutubisho vinavyohitajika na mazao.

Teknolojia hii pia huchangia katika kupunguza uzalishaji wa gesi joto kwa kupunguza shughuli za mara kwa mara za kulima ambazo huongeza utoaji wa hewa ya ukaa kutoka ardhini. Kwa kufanya hivyo, kilimo hifadhi kinakuwa sehemu ya juhudi za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Vilevile, mfumo huu huongeza uwepo wa viumbe hai wenye manufaa kwenye udongo kama vile minyoo na vimelea mbalimbali vinavyosaidia kuvunjavunja mabaki ya mimea na kuongeza rutuba ya udongo. Hali hii hujenga mfumo wa ikolojia wenye afya na unaosaidia uzalishaji endelevu wa mazao.

Kwa ujumla, kilimo hifadhi ni teknolojia muhimu inayowezesha uzalishaji wa mazao kwa njia endelevu huku ikihifadhi mazingira. Matumizi yake yanaweza kusaidia wakulima kuongeza tija, kuhifadhi rutuba ya udongo, kutumia maji kwa ufanisi na kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi.

Hivyo, kuendelea kuhamasisha matumizi ya kilimo hifadhi ni hatua muhimu katika kujenga sekta ya kilimo yenye ushindani, tija na inayolinda mazingira kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.



***Teknolojia ya kilimo hifadhi huongeza matumizi bora ya maji na kuboresha afya ya udongo kwa uzalishaji endelevu.***



# UJENZI WA KITUO CHA BIOSCIENCE KUANZA RASMI MKOANI MOROGORO

**TAASISI** ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) inatarajia kuanza ujenzi wa maabara ya kibayolojia (Bioscience) katika Kijiji cha Wami Sokoine, Kata ya Dakawa, Wilaya ya Mvomero mkoani Morogoro.

Hatua hiyo imekuja baada ya TARI kufanya makabidhiano rasmi ya eneo la ujenzi wa Kituo cha Bioscience kwa mkandarasi mjenzi, China Railway Seventh Group (CRSG), hatua inayofungua rasmi utekelezaji wa mradi huo muhimu wa kisayansi na utafiti nchini.

Makabidhiano hayo yalifanyika Mei 15, 2026 katika eneo la mradi katika hafla ambayo mkandarasi mjenzi alikabidhiwa michoro na ramani za majengo mbalimbali yatakayojengwa katika kituo hicho kutoka kwa mkandarasi mshauri, K & M Company ili kuanza rasmi kazi za ujenzi.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali akiwemo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, Mhe. Paulo Faty, Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dkt. Thomas Bwana, Diwani wa Kata ya Dakawa, Mhe. Joshua Lugaso, viongozi kutoka TARI Makao Makuu, wafanyakazi wa taasisi hiyo pamoja na wananchi wa maeneo yanayozunguka mradi huo.

Akizungumza katika hafla hiyo, Dkt. Bwana aliishukuru Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero kwa kuipatia TARI eneo la kutekeleza mradi huo mkubwa wa kimkakati na kuongeza kuwa kukamilika kwa Kituo cha Bioscience kutaimarisha uwezo wa nchi katika kufanya tafiti za kisasa na kutoa huduma za maabara kwa kiwango cha kimataifa.

Aliongeza kuwa kituo hicho kinatarajiwa kutumiwa si tu na TARI bali pia na taasisi nyingine za utafiti ndani na nje ya Tanzania, hivyo kuongeza ushirikiano wa kisayansi na kuimarisha mchango wa utafiti katika maendeleo ya sekta ya kilimo na uchumi wa taifa.

Kwa upande wake, Msanifu Majengo kutoka kampuni ya mkandarasi mshauri, Bw. Albert Mwambafu, alisema kuwa pamoja na maabara za kisasa, mradi huo utahusisha ujenzi wa miundombinu mingine muhimu ikiwemo nyumba za wafanyakazi, majengo ya huduma za kijamii, maeneo ya mapumziko, karakana na huduma nyingine za msingi zitakazowezesha kituo hicho kufanya kazi kwa ufanisi.

Ujenzi wa Kituo cha Bioscience unatarajiwa kuwa chachu ya kuimarisha tafiti za kibayolojia na teknolojia za kisasa za kilimo nchini, sambamba na kuongeza uwezo wa Tanzania katika kukabiliana na changamoto mbalimbali za uzalishaji wa mazao na usalama wa chakula.





# PROF. MSOFFE ATEMBELEA TARI-UYOLE, ASISITIZA UMUHIMU WA UTAFITI NA UBUNIFU WA KILIMO

**NAIBU** Katibu Mkuu anayeshughulikia Maendeleo ya Mazao na Usalama wa Chakula, Wizara ya Kilimo Prof. Peter Msoffe, ametembelea Kituo cha TARI-Uyole kilichopo mkoani Mbeya na kuwataka watafiti kituoni hapo kuongeza juhudi katika kufanya tafiti na kuwa wabunifu ili kuzalisha teknolojia na bunifu zinazoweza kuongeza tija, uzalishaji na ushindani katika sekta ya kilimo.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo iliyofanyika Mei 4, 2026, Prof. Msoffe alieleza kuwa utafiti unaofanywa na TARI una mchango mkubwa katika kutatua changamoto zinazowakabili wakulima na kuhakikisha upatikanaji wa teknolojia sahihi zinazochochea maendeleo ya kilimo na kuimarisha usalama wa chakula nchini.

Katika hatua nyingine, Prof. Msoffe alikumbusha umuhimu wa kudumisha mahusiano mazuri na ushirikiano miongoni mwa watumishi mahali pa kazi, akieleza kuwa wafanyakazi hutumia sehemu kubwa ya muda wao kazini kuliko kwenye makazi yao, hivyo mazingira bora na rafiki ya kazi ni msingi muhimu wa kuongeza ufanisi na tija katika utekelezaji wa majukumu yao.






Aidha, Prof. Msoffe alitembelea Uwanja wa Maonesho ya Kilimo ya Nane Nane wa John Mwakangale jijini Mbeya kukagua maendeleo ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali inayotekelezwa katika eneo hilo kwa ajili ya kuboresha mazingira ya maonesho na huduma kwa wadau wa sekta ya kilimo. Ziara hiyo ni sehemu ya juhudi za Wizara ya Kilimo za kufuatilia utekelezaji wa shughuli za utafiti, ubunifu na maendeleo ya miundombinu inayolenga kuimarisha mchango wa sekta ya kilimo katika ukuaji wa uchumi na ustawi wa wananchi.

Akiwa katika kituo cha TARI – Uyole Prof. Msoffe alipokelewa na Mkurugenzi wa kituo hicho, Dkt. Emmanuel Mrema, na kufanya mazungumzo na Menejimenti ya kituo hicho kuhusu shughuli mbalimbali za utafiti na maendeleo ya kilimo.



# WAKULIMA ARUSHA WASHIRIKISHWA KATIKA TATHMINI ZA UTAFITI WA MBEGU ZA MAHARAGE

**KITUO** cha TARI Selian kwa kushirikiana na wakulima kutoka Kijiji cha Nadosoito, Kata ya Murieti, Wilaya ya Arusha, imeendesha zoezi la tathmini ya majaribio ya aina sita za mbegu za maharage zinazofanyiwa utafiti katika kituo hicho.

Zoezi hilo ambalo limefadhiliwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) linalenga kuhakikisha kuwa mbegu zinazotafitiwa zinakidhi mahitaji halisi ya wakulima na soko. Katika tathmini hiyo, wakulima walipata fursa ya kutathmini aina mbalimbali za mbegu kwa kuzingatia sifa muhimu ikiwemo ustahimilivu wa ukame, magonjwa na wadudu, muda wa kukomaa, kiwango cha uzalishaji pamoja na uhakika wa soko.

Jumla ya wakulima 15, wakiwemo wanawake saba na wanaume wanane kutoka Kijiji cha Nadosoito, walishiriki katika zoezi hilo na kutoa maoni yao kuhusu aina za mbegu zilizowasilishwa. Maoni hayo yanatarajiwa kusaidia watafiti katika mchakato wa kuboresha na kupata mbegu bora zitakazoongeza tija kwa wakulima na kukidhi mahitaji ya walaji.

Akizungumza wakati wa tathmini hiyo, Mratibu wa Uhaulishaji Teknolojia na Mahusiano wa Kituo cha TARI Selian, Dkt. Edith Kadege, aliwashukuru wakulima kwa kujitokeza na kushiriki kikamilifu katika zoezi hilo na kuongeza kuwa ushiriki wa wakulima katika tafiti ni muhimu kwa kuwa unasaidia kupata teknolojia zinazokubalika na watumiaji wa mwisho, huku ukiwajengea uwezo wa kufanya uchaguzi sahihi wa mbegu kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na kipato.

Kwa upande wao, wakulima walikipongeza Kituo cha TARI Selian kwa kuendelea kuwashirikisha katika shughuli za utafiti zinazohusu mazao wanayolima. Walisema ushirikishwaji huo unawapa nafasi ya kutoa maoni yanayozingatiwa katika maendeleo ya teknolojia za kilimo na kuchangia upatikanaji wa mbegu bora zinazoweza kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi.

Wakulima hao walieleza kuwa ushirikiano kati ya watafiti na wakulima ni nguzo muhimu katika kuimarisha kilimo chenye tija, kuongeza usalama wa chakula na kuboresha maisha ya jamii za vijijini. Zoezi hilo linaonesha dhamira ya TARI ya kuhakikisha teknolojia za kilimo zinazoendelezwa zinajibu mahitaji ya wakulima na kuchangia maendeleo endelevu ya sekta ya kilimo nchini.



8 Jumatatu Juni 1 - 7, 2026 Makala Rada | Rada Makala Jumatatu Juni 1 - 7, 2026 9

# TARI na mapinduzi ya kilimo kidijitali

Na Mussa Mkama




Dkt. Thomas Bwana

HABARILEO JUMANNE JUNI 2, 2026 MAKALA 11

KILIMO SHADIDI CHA MPUNGA

# Kielelezo kazi za watafiti zinavyogusa wakulima



Maelezo



# Teknolojia ya TARI Yawa Mkombozi wa Wakulima wa Mpunga Kilosa

Na Maria Paul - TARI

Wakulima wa zao la mpunga wilayani Kilosa, mkoa wa Morogoro wamehimizwa kuachana na kilimo cha mazoea na kuzingatia matumizi ya teknolojia ya kilimo shadidi cha mpunga inayotajwa kuongeza mavuno kwa gharama ndogo na matumizi madogo ya maji na mbegu.

Rai hiyo imetolewa kwa wakulima imetolewa hivi karibuni na Mtafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Dkt. Atugonza Bilaro, wakati wa siku ya mkulima wa mpunga iliyofanyika katika skimu ya Ilongailiyopo wilayani Kilosa.

Dkt. Bilaro amesema teknolojia ya kilimo shadidi imeendelea kuleta mapinduzi katika uzalishaji wa mpunga kutokana na uwezo wake wa kuongeza tija huku ikiwasaidia wakulima kupunguza gharama za uzalishaji shambani.

Amesema tofauti na kilimo cha mazoea, mfumo huo unahusisha matumizi ya mbegu kidogo, nafasi maalum ya upandaji pamoja na usimamizi mzuri wa maji jambo linalowezesha mimea kukua vizuri na kutoa mavuno mengi zaidi.

"Lengo la TARI ni kuhakikisha wakulima wengi zaidi wanapata elimu ya kilimo bora ili kuongeza uzalishaji wa chakula na kuimarisha kipato cha kaya zinazotegemea zao la mpunga nchini",alisema Bilaro

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Afisa Tarafa ya Kimamba, Bi. Sabina Lucas ameipongeza TARI kwa kuendelea kuwafikia wakulima kupitia mafunzo ya vitendo yanayosaidia kuongeza uelewa wa mbinu bora za kisasa za kilimo.

Alisema zaidi ya wakulima 4,000 katika maeneo mbalimbali yanayolima mpunga wamefikiwa na elimu hiyo, hatua ambayo imeanza kuleta matumaini mapya kwa wakulima wengi wanaotafuta njia bora za kuongeza uzalishaji.

Mkulima wa Skimu ya Ilonga, Alex Mwinuka alisema kabla ya kupata mafunzo hayo alikuwa akitumia zaidi ya kilogramu 10 za mbegu kupanda ekari moja, lakini sasa anatumia kilogramu mbili pekee kupitia mfumo wa kitalu mkeka uliotolewa na wataalamu wa TARI.

Naye Godfrey Paschal alisema awali alikuwa akivuna wastani wa gunia nane hadi 10 kwa ekari kupitia kilimo cha kawaida, lakini baada ya kuanza kutumia kilimo shadidi sasa anapata kati ya gunia 30 hadi 35 kwa ekari, hali inayodhihirisha mafanikio ya teknolojia hiyo katika kuongeza uzalishaji na kipato cha wakulima.

Nchi Yetu Online | 06
www.maelezo.go.tz

# TARI YASHIRIKI ZIARA YA MAFUNZO NA KUBADILISHANA UZOEFU KUHUSU ZANA ZA KILIMO NCHINI UFILIPINO




**TAASISI** ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO) imeshiriki ziara ya mafunzo na kubadilishana uzoefu kuhusu zana za kilimo nchini Ufilipino kuanzia Mei 5 hadi 7, 2026.

Ziara hiyo iliyofanyika katika Kituo cha Maendeleo ya teknolojia za baada ya Mavuno na Zana za Kilimo cha nchini Ufilipino (PHilMech) imelenga kujifunza na kubadilishana uzoefu kuhusu matumizi ya teknolojia za kisasa katika kuongeza tija ya kilimo, kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno na kuboresha huduma za zana bora za kilimo kwa wakulima.

Katika ziara hiyo, wataalamu kutoka TARI wakiongozwa na Mkurugenzi Mkuu Dkt. Thomas Bwana walipata fursa ya kujifunza kuhusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya zana za kilimo, usambazaji wa mashine za kilimo, utoaji wa mafunzo kwa wakulima pamoja na mifumo ya usimamizi wa teknolojia za kilimo.

Aidha, ujumbe huo pia ulitembelea Taasisi ya Utafiti wa Mpunga ya Ufilipino pamoja na kampuni zinazozalisha mashine za kilimo kwa lengo la kujionea maendeleo ya teknolojia na ubunifu unaotumika katika kuongeza uzalishaji na uongezaji thamani wa mazao baada ya mavuno.



Ushiriki wa TARI katika ziara hiyo unaendelea kuimarisha ushirikiano wa kimataifa katika sekta ya kilimo na kusaidia upatikanaji wa maarifa na teknolojia zitakazochangia maendeleo ya kilimo nchini Tanzania.

Wadau wengine walioshiriki katika ziara hiyo ni mwakilishi IMARA TECH, Mhandisi kilimo kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, Mkulima kiongozi kutoka Morogoro, Mhandisi kutoka Wizara ya Kilimo, CAMARTEC pamoja na FAO.



# WAKULIMA WA SOYA MKOANI IRINGA KUNUFAIKA NA KILIMO HIFADHI

**TAASISI** ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kupitia Kituo cha Utafiti wa Kilimo Kifyulilo, kwa kushirikiana na Umoja wa Kimataifa wa Uhifadhi wa Asili (IUCN) wametoa mafunzo kuhusu kilimo hifadhi kwa wakulima wa zao la soya mkoani Iringa, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kuimarisha uzalishaji endelevu na kuhifadhi mazingira.

Mafunzo hayo yalifanyika kuanzia Mei 5 hadi 8, 2026 kupitia Mradi wa RESET (Restoration of Ecosystem Services and Environmental Sustainability in Tanzania), unaolenga kuimarisha huduma za mifumo ya ikolojia na kukuza uendelevu wa mazingira kupitia sekta ya kilimo.

Katika mafunzo hayo, wakulima walipatiwa elimu kuhusu mnyororo mzima wa thamani wa zao la soya, kuanzia matumizi ya mbegu bora na mbinu za kisasa za uzalishaji, udhibiti wa magonjwa na wadudu waharibifu, mbinu bora za uvunaji, uhifadhi na usindikaji wa mazao ili kuongeza thamani na kipato cha kaya.

Aidha, washiriki walijengewa uwezo kuhusu kanuni na mbinu za kilimo hifadhi, zikiwemo uhifadhi wa maji na udongo, matumizi endelevu ya ardhi, pamoja na njia za kupunguza mmomonyoko wa udongo na kulinda rutuba ya ardhi. Mafunzo hayo pia yalisisitiza umuhimu wa kulinda mifumo ya ikolojia ya kilimo ili kuhakikisha uzalishaji unaendelea kuwa endelevu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Jumla ya wakulima 427 kutoka vijiji 12 vya Wilaya za Iringa na Kilolo walinufaika na mafunzo hayo. Kati yao, wanawake walikuwa asilimia 52.9 ya washiriki wote, jambo linaloonesha mafanikio ya juhudi za kuwawezesha wanawake kushiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji na maendeleo ya kilimo.



Akizungumzia mafanikio ya mafunzo hayo, Mratibu wa Uhaulishaji wa Teknolojia na Mahusiano wa TARI, Bi. Lilian Ngusi, kwa kushirikiana na Mkuu wa Sehemu ya Uhaulishaji Teknolojia wa kituo cha TARI Kifyulilo, Bw. Moses Mkumbo, walieleza kuwa ushirikiano kati ya TARI na IUCN umeendelea kuwa nguzo muhimu katika kufikisha teknolojia na maarifa ya kisasa kwa wakulima.

Walisema TARI itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo ili kuongeza kasi ya usambazaji wa teknolojia za kilimo, kuimarisha matumizi ya mbinu za kilimo hifadhi na kuongeza tija ya mazao, sambamba na kuboresha maisha ya wakulima na kuchangia uhifadhi wa mazingira nchini.

Mafunzo hayo yanaonesha dhamira ya TARI ya kuhakikisha tafiti na teknolojia za kilimo zinawafikia wakulima kwa wakati, huku zikichangia katika kujenga sekta ya kilimo yenye tija, inayohimili athari za mabadiliko ya tabianchi na kulinda rasilimali za asili kwa maendeleo endelevu.



# TARI-HOMBOLO, CIMMYT KUTATHMINI MAENDELEO YA MAJARIBIO YA MIUNDOMBINU YA UTAFITI

**KITUO** Mahiri cha Utafiti wa Mazao ya Nyanda Kame cha TARI-Hombolo kilichopo jijini Dodoma pamoja na watafiti wa Shirika la Kimataifa la Uboreshaji wa Mahindi na Ngano (CIMMYT) wamekutana kutathmini maendeleo ya majaribio ya utafiti yanayoendelea pamoja na kukagua miundombinu ya kituo hicho.

Ziara hiyo ya kikazi iliyofanyika Mei 6, 2026 katika kituo cha TARI-Hombolo ilihusisha ugeni kutoka CIMMYT: Dkt. Happy Daudi, Harish Gandhi na Janet Kimonye. Kwa upande wa TARI: Dkt. Andekelile Mwamahonje, Devotha Mchau na David Mache.

Lengo kuu la ziara hiyo ni kutathmini maendeleo ya majaribio mbalimbali ya utafiti yanayotekelezwa katika kituo hicho pamoja na kufanya ukaguzi wa miundombinu inayotumika katika shughuli za utafiti.

Ugeni huo ukiwa katika Kituo cha TARI-Hombolo ulipata wasilisho kutoka kwa Meneja wa Kituo Dkt. Emmanuel Chilagane kuhusu shughuli za utafiti, miradi mbalimbali inayotekelezwa kituoni hapo pamoja na mafanikio yaliyofikiwa. Aidha,



Dkt. Eliud Kongola (CRI) aliwaongoza wageni hao kutembelea majaribio ya utafiti na miundombinu mbalimbali ya kituo huku akitoa maelezo kuhusu maendeleo na matumizi yake katika kuendeleza tafiti za kilimo cha mazao ya nyanda kame.

Kwa upande wake Harish Gandh kutoka CIMMYT aliipongeza TARI-Hombolo kwa juhudi kubwa zinazofanyika katika kutekeleza tafiti zenye tija kwa wakulima, hususan katika maendeleo ya teknolojia za mazao ya nyanda kame, na kueleza kuridhishwa na hatua zilizofikiwa katika majaribio pamoja na hali ya miundombinu iliyopo kituoni hapo.



# TARI-UYOLE, CIMMYT KUFUATILIA MAJARIBIO YA KIKANDA NA MIUNDOMINU YA UTAFITI WA MBEGU

**KITUO** cha TARI Uyole pamoja na Kituo cha Kimataifa cha Kuboresha Mahindi na Ngano (CIMMYT) wamekutana tarehe 21 Mei, 2026 kwa lengo la kufuatilia na kutathmini maendeleo ya majaribio ya kikanda (Regional Trials) pamoja na miundombinu ya utafiti wa mbegu (Breeding Infrastructure) kwa ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini (ESA). Majaribio hayo yanahusisha mazao ya mtama, ulezi na uwele yanayofanyiwa utafiti katika kituo hicho.

Ugeni huo uliongozwa na Bw. Tamerlane Mark Nas, Mkuu wa Programu za Uzalishaji wa Mbegu za mazao ya mtama, ulezi na uwele kutoka CIMMYT kwa ukanda wa ESA ambae alifuatana na watafiti Bw. Lloyd Mbulwe kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zambia (ZARI) na Bw. Jared Onduso kutoka CIMMYT Kenya. Aidha, katika ziara hiyo walikuwepo pia Dkt. Eliud Kongola na Dkt. Andekelile Mwamahonja kutoka TARI.

Ugeni huo ulipokelewa na Mkurugenzi wa Kituo cha TARI-Uyole, Dkt. Emmanuel Mrema, ambaye aliwaongoza wageni hao kutembelea maeneo mbalimbali ya utafiti yakiwemo mashamba ya



majaribio. Ugeni huo ulipokea taarifa ya utafiti kutoka kwa Dkt. Dennis Tippe kuhusu maendeleo ya tafiti za mazao ya mtama, ulezi na uwele, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika hatua mbalimbali za utafiti.

Mbali na kutembelea majaribio ya shambani (field trials), wageni hao walitembelea pia vitalu nyumba (screen houses) vilivyopo kituoni hapo na kujionea shughuli mbalimbali za utafiti zinazoendelea. Vilevile, walikagua maendeleo ya ujenzi wa kitalu nyumba kipya kinachotarajiwa kuimarisha uwezo wa kituo katika kutekeleza tafiti za uzalishaji na uboreshaji wa mbegu.

Akizungumza baada ya ziara hiyo, Bw. Tamerlane Mark Nas aliipongeza timu ya watafiti na wataalamu wa TARI kwa juhudi, maarifa na weledi walioouonyesha katika utekelezaji wa majaribio hayo. Alieleza kuridhishwa na maendeleo ya kazi na kusisitiza kuwa CIMMYT itaendelea kushirikiana na TARI katika kuendeleza tafiti zenye manufaa kwa wakulima na sekta ya kilimo kwa ujumla.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa TARI-Uyole, Dkt. Emmanuel Mrema, aliushukuru ugeni huo kwa kutembelea kituo hicho na kwa ushirikiano unaoendelea kati ya TARI na CIMMYT. Alisisitiza kuwa ushirikiano huo ni muhimu katika kuimarisha tafiti za mazao ya nafaka yanayostahimili mabadiliko ya tabianchi na kuongeza tija kwa wakulima wa Tanzania na ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini.






# TARI YASHIRIKI MAONESHO YA PAMOJA YA BIASHARA YA TANZANIA NA BURUNDI

**TAASISI** ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imeshiriki katika maonesho ya pamoja ya biashara ya Tanzania na Burundi yaliyofanyika kuanzia tarehe 21 hadi 24 Mei 2026, yakiwa na lengo la kuimarisha ushirikiano wa kibiashara, uwekezaji na maendeleo ya sekta ya kilimo kati ya nchi hizo mbili.

Maonesho hayo yalifunguliwa rasmi na Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara ya Burundi, Ndg. Nibigira Christine, ambaye alikuwa mgeni rasmi. Hafla hiyo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali, sekta binafsi na wadau wa biashara kutoka Tanzania na Burundi, wakijadili fursa za biashara na uwekezaji zinazoweza kuchochea maendeleo ya kiuchumi katika ukanda huo.

Kwa upande wa Tanzania, viongozi waliohudhuria ni pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Mhe. Simon



Sirro, Balozi wa Tanzania nchini Burundi, Ndg. Gelasius Byakanwa, mwakilishi wa Waziri wa Viwanda na Biashara Tanzania pamoja na viongozi wengine kutoka serikalini na sekta binafsi. Upande wa Burundi uliwakilishwa pia na Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara na Wenye Viwanda Burundi (Burundi Chamber of Commerce and Industry) na mwakilishi wa Gavana wa Mkoa husika.

Kupitia maonyesho hayo, TARI ilipata fursa ya kuonesha na kutangaza teknolojia mbalimbali za kilimo zilizobuniwa na taasisi hiyo kwa lengo la kuongeza uzalishaji na tija katika sekta ya kilimo. Wageni waliotembelea banda la TARI walipata elimu kuhusu teknolojia na ubunifu unaochangia kukabiliana na changamoto za uzalishaji, kuongeza thamani ya mazao na kuimarisha usalama wa chakula.

Ushiriki wa TARI katika maonyesho hayo umeendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda katika sekta ya kilimo, biashara na uwekezaji, huku ukifungua fursa mpya za usambazaji wa teknolojia za kilimo na kubadilishana uzoefu kati ya Tanzania na Burundi. Hatua hiyo inachangia juhudi za kukuza uchumi wa wananchi wa nchi hizo mbili kupitia maendeleo endelevu ya sekta ya kilimo.




# TARI, TAWIRI KUIMARISHA USHIRIKIANO WA KITAFITI

**TAASISI** ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI) zimeonesha dhamira ya kuimarisha ushirikiano katika maeneo mbalimbali ya utafiti na maendeleo kwa lengo la kuchangia maendeleo endelevu ya sekta za kilimo, mazingira na uhifadhi wa maliasili nchini.

Hayo yamebainika Mei 19, 2026, wakati Mkurugenzi Mkuu wa TAWIRI, Dkt. Eblate Mjingo, alipotembelea Ofisi za TARI Makao Makuu jijini Dodoma na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dkt. Thomas Bwana. Mazungumzo hayo yalijikita katika kubaini maeneo ya kimkakati ya ushirikiano wa kitafiti kati ya taasisi hizo mbili.

Miongoni mwa maeneo yaliyojadiliwa ni utekelezaji wa tafiti zinazohusu wanyamapori, viumbe vamizi vinavyosababisha madhara kwa mazingira, uchumi na jamii, pamoja na kutafuta suluhisho la changamoto ya mwingiliano kati ya binadamu na wanyamapori ambayo imeendelea kuathiri shughuli za uzalishaji katika baadhi ya maeneo nchini.

Aidha, taasisi hizo zimejadili uwezekano wa kufanya tafiti za pamoja kuhusu mimea na mazao ambayo hayashambuliwi au kuharibiwa kwa urahisi na wanyamapori. Tafiti hizo zinatarajiwa kusaidia kupunguza hasara kwa wakulima, kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao ya kilimo na kuchangia juhudi za uhifadhi wa mazingira na wanyamapori.




Katika ziara hiyo, Dkt. Mjingo alipata fursa ya kutembelea shamba la zabibu la TARI Makutupora pamoja na eneo la uzalishaji wa mvinyo, ambapo alijionea shughuli mbalimbali za utafiti, ubunifu na uongezaji thamani wa mazao zinazotekelezwa na TARI kwa lengo la kuendeleza sekta ya kilimo nchini.

Pia, alipata nafasi ya kukutana na Mkurugenzi wa Uhawilishaji Teknolojia na Mahusiano wa TARI, Dkt. Sophia Kashenge, pamoja na Kaimu Mkurugenzi wa Kituo cha TARI Makutupora, Isack Teya, ambapo walibadilishana uzoefu na kujadili fursa za kuendeleza ushirikiano katika nyanja za utafiti, ubunifu na uhawilishaji wa teknolojia.

Ushirikiano huo unatarajiwa kuimarisha matumizi ya sayansi na teknolojia katika kutatua changamoto zinazokabili sekta za kilimo na uhifadhi wa maliasili, huku ukichangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini.



# TARI, WADAU WAJADILI USHIRIKIANO KUKUZA KILIMO CHA MHOGO

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Chuo Kikuu cha Cornell pamoja na Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo cha Kitropiki (IITA) wamekutana kwa pamoja kwa lengo la kuimarisha ushirikiano katika maendeleo ya kilimo cha mhogo nchini Tanzania.

Wadau hao wamekutana Mei 14, 2026 Makao Makuu ya TARI jijini Dodoma, ambapo walipata fursa ya kujionea mafanikio ya utekelezaji wa Mradi wa Mhogo Bora unaotekelezwa kwa ushirikiano kati ya TARI, Chuo Kikuu cha Cornell na IITA.

Mradi huo unaofadhiliwa na Chuo Kikuu cha Cornell na kuratibiwa na IITA kwa kushirikiana na TARI unatekelezwa katika mikoa ya Tabora, Kigoma, Katavi, Singida na Rukwa lengo likiwa kuhamasisha matumizi ya mbegu bora za mhogo zinazostahimili magonjwa ya virusi, kuendeleza mbinu bora za uzalishaji na kuongeza kipato cha wakulima wadogo, sambamba na kuimarisha usalama wa chakula na kupunguza uhaba wa mbegu bora nchini.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dkt. Thomas Bwana, alisema taasisi itaendelea kuwekeza katika utafiti wa kisasa na kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali, ikiwemo sekta binafsi, ili kuhakikisha wakulima wanapata mbegu bora kwa wakati na kwa urahisi.



Kwa upande wake, Mwakilishi wa IITA ambaye pia ni Mtaalamu Mshauri wa Mifumo ya Mbegu, Dkt. Kiddo Julius Mtunda, akiwa ameambatana na Prof. Hale Ann Tufan kutoka Chuo Kikuu cha Cornell pamoja na Prof. Chiedozie Egesi kutoka Taasisi ya Kitaifa ya Utafiti wa Mazao ya Mizizi ya Umudike nchini Nigeria, alisema mradi huo umefanikiwa kusambaza vipande milioni 1.9 vya mbegu mama za mhogo kwa kushirikiana na TARI.

Alibainisha kuwa kupitia mradi huo, takribani wakulima 3,996 wamenufaika moja kwa moja, huku zaidi ya shule 12 za msingi katika maeneo yanayotekelezwa mradi huo zikiendelea kunufaika kupitia uboreshaji wa lishe kwa wanafunzi.

Baada ya kikao hicho, ugeni huo ulitembelea Kituo cha TARI Makutopora na kujionea shughuli mbalimbali za utafiti wa zao la zabibu pamoja na maendeleo ya teknolojia za uongezaji thamani kupitia kiwanda kidogo cha usindikaji kilichopo kituoni hapo.

Kaimu Mkurugenzi wa Kituo cha TARI Makutopora, Mtafiti Isack Teya, alitoa maelezo kuhusu aina mbalimbali za zabibu zinazolimwa kituoni hapo, matumizi yake, pamoja na mchakato wa uzalishaji wa mvinyo bora unaofanyika katika kituo hicho.



# TARI YASHIRIKI WARSHA YA KIMATAIFA KUONGEZA THAMANI YA TAFITI ZA KILIMO AFRIKA

**TAASISI** ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imeshiriki katika warsha ya kimataifa iliyofanyika tarehe 03 Juni, 2026 jijini Arusha ikilenga kuongeza thamani ya matokeo ya tafiti za kilimo barani Afrika kupitia ushirikiano na sekta binafsi.

Warsha hiyo imewakutanisha wadau kutoka mashirika ya maendeleo, taasisi za utafiti na sekta binafsi kutoka ndani na nje ya Afrika, kwa lengo la kujadili mbinu bora za kuimarisha ushirikiano katika biashara, ubunifu na matumizi ya matokeo ya tafiti za kilimo. Mjadala mkuu ulijikita katika kuhakikisha tafiti zinazofanyika zinawafikia walengwa na kuchangia moja kwa moja katika kuongeza tija, usalama wa chakula na ushindani wa sekta ya kilimo.

Akizungumza katika warsha hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa TARI Dkt. Thomas Bwana alieleza kuwa mafanikio ya Dira 2050 yanategemea uwekezaji thabiti katika tafiti, ubunifu na teknolojia huku akibainisha kuwa changamoto kubwa si upungufu wa tafiti, bali ni kiwango cha matumizi ya matokeo yake ambacho bado hakijafikia matarajio.



Kwa upande wake, Godfrey Moshi, ambaye ni Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Uendeshaji wa Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo kutoka Idara ya Mafunzo ya Kilimo na Utafiti Wizara ya Kilimo, amesema Serikali inaendelea kuimarisha uwekezaji katika tafiti na ubunifu ili kuongeza tija katika sekta ya kilimo nchini.

Ameongeza kuwa ni muhimu kwa sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika kufadhili tafiti na kuendeleza matumizi ya teknolojia bunifu zinazotokana na utafiti, hatua itakayosaidia kuongeza uzalishaji, kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kuboresha masoko ya mazao.

Warsha hiyo ya siku tatu ilikuwa na lengo la kutoa mapendekezo muhimu kuhusu namna ya kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi za utafiti na sekta binafsi, kulinda hakimiliki za ubunifu, pamoja na kuharakisha matumizi ya matokeo ya tafiti kwa maendeleo endelevu ya kilimo barani Afrika.

Pamoja na warsha hiyo kulikuwa na maonesho ya bidhaa mbalimbali zilizoongezewa thamani kutoka kwa wadau na taasisi mbalimbali ikiwemo TARI.






# TARI NA TCB KUIMARISHA UTAFITI NA KUKUZA SEKTA YA KAHAWA NCHINI

**TAASISI** ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) na Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB) wamekutana katika kikao cha pamoja kilicholenga kujadili maendeleo ya utafiti wa zao la kahawa, kuimarisha ushirikiano wa kitaasisi na kuweka mikakati thabiti ya kukuza sekta ya kahawa nchini.

Kikao hicho kilichofanyika tarehe 28 Mei 2026 katika Makao Makuu ya Bodi ya Kahawa Tanzania, jijini Moshi Mkoani Kilimanjaro, kilitoa fursa kwa wajumbe kubadilishana taarifa kuhusu mafanikio ya shughuli mbalimbali zinazolenga kuongeza uzalishaji, kuboresha ubora na kuongeza thamani ya zao la kahawa nchini.

Aidha, viongozi wa taasisi hizo walisisitiza umuhimu wa kuimarisha ushirikiano wa karibu kati ya taasisi za utafiti na wadau wa sekta ya kahawa, wakibainisha kuwa hatua hiyo ni muhimu katika kuongeza tija kwa wakulima, kuboresha huduma za utafiti na kuongeza ushindani wa kahawa ya Tanzania katika soko la kimataifa, sambamba na kuendeleza mchango wa sekta hiyo katika uchumi wa taifa.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dkt. Thomas Bwana aliambatana na Meneja wa Kituo cha TARI TaCRI Dkt. Suzan Mbwambo katika kikao.

Kituo cha TARI TaCRI ndicho chenye jukumu kitaifa la utafiti wa zao la Kahawa nchini.



TARI
UNA MAONI GANI KUHUSU HUDUMA ZETU?
tari.tanzania TARI Tanzania TanzaniaTari TARITanzania



# TARI NA TAHA ZAJADILI KUIMARISHA USHIRIKIANO WA KIMKAKATI KATIKA UTAFITI NA UBUNIFU WA KILIMO CHA MBOGA



**MKURUGENZI** Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Dkt. Thomas Bwana na Mtendaji Mkuu wa TAHA, Dkt. Jacqueline Mkindi wamefanya kikao kazi cha kuweka mikakati madhubuti ya kuimarisha zaidi ushirikiano wa kimkakati kati ya TARI na TAHA.

Mazungumzo hayo yalilenga kuboresha maeneo mbalimbali ya utafiti wa kilimo ikiwemo uboreshaji wa utafiti wa mbegu za mazao ya bustani ili kuhakikisha upatikanaji wa mbegu bora zinazokidhi viwango vya soko la ndani na la kimataifa.

Aidha, viongozi hao walisisitiza umuhimu wa kuendeleza ushirikiano huo ili kuongeza tija, ushindani na ukuaji endelevu wa sekta ya mazao ya bustani nchini na kuongeza kuwa ushirikiano huo utachangia kuwawezesha wakulima kupata teknolojia bunifu, mbegu bora na huduma za kitaalamu zitakazochochea maendeleo ya sekta ya kilimo na uchumi wa Taifa kwa ujumla.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI aliambatana na Meneja wa kituo cha TARI Tengeru, Dkt. Happiness Mollel katika kikao hicho.

Kituo cha TARI Tengeru ndicho chenye jukumu kitaifa la utafiti wa mazao ya Bustani nchini.




*Watumishi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) wakiwa katika picha ya pamoja katika Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani.*

*Waziri wa Kilimo, Mhe. Daniel Chongolo (Mb) (katikati), akizindua pikipiki za Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) zilizotolewa kwa ajili ya kuimarisha utekelezaji wa shughuli za utafiti, ugani na usambazaji wa teknolojia za kilimo kwa wakulima nchini.*






*Watumishi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) wakishiriki Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi), wakionesha mshikamano na kutambua mchango wa wafanyakazi katika maendeleo ya sekta ya kilimo na Taifa kwa ujumla*



WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
TARI
HERI YA SIKUKUU YA MUUNGANO
26 Aprili
"Miaka 62 ya Muungano: Amani, Umoja na Mshikamano ni Msingi wa Maendeleo Endelevu"
TARI- Utafiti kwa Maendeleo ya Kilimo
Tufuatilie
TARI Tanzania
tari.tanzania
TanzaniaTari




WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
TARI
HERI YA SIKU YA WAFANYAKAZI
CENTRAL AGRICULTURE LABORATORY
"Kazi zenye staha ni nguzo imara kwa maendeleo endelevu katika utekelezaji wa Dira ya Taifa 2050"
TARI- Utafiti kwa Maendeleo ya Kilimo
Tufuatilie
TARI Tanzania
tari.tanzania
TanzaniaTari
TARI Tanzania




WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
TARI
Eid Al-Adha
MUBARAK
Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Watumishi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) tunawatakia
Heri ya Sikukuu ya Eid al - Adha
TARI - Utafiti kwa Maendeleo ya Kilimo
Tufuatilie
TARI Tanzania
tari.tanzania
TanzaniaTari
TARI Tanzania




WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
TARI
KUPAMBANA NA TINDIKALI
Je shamba lako lina tindikali?
Achana na kilimo cha mazoea.Pima afya ya udongo sasa ili utambue aina na viwango stahili vya mbolea shambani kwako kwa kilimo chenye tija na endelevu. Tumia klinik za udongo za TARI kupima afya ya shamba lako na kuongeza mavuno na kipato.
Ardhi yenye tindikali husababisha upungufu wa mavuno kwa zaidi ya asilimia 50.
#DIRA2050
Tufuatilie
tari.tanzania
Tari Tanzania
TanzaniaTari
TARI TANZANIA
Utafiti kwa Maendeleo ya Kilimo




MAADHIMISHO YA WIKI YA
MAZINGIRA DUNIANI 2026
"Mazingira ni uhai wa kilimo chetu. Tuhifadhi udongo, vyanzo vya maji na misitu ili kuongeza uzalishaji na kuhakikisha usalama wa chakula kwa taifa letu. Wiki ya Mazingira 2026 - Kilimo endelevu, maisha endelevu."
01 - 06 JUNI 2026
JAKAYA KIKWETE CONVENTION CENTER




# TARI MARATHON - 2026

# MIAKA 10 YA TARI: UTAFITI, USAMBAZAJI WA TEKNOLOJIA NA USHAWISHI WA SERA KWA KILIMO ENDELEVU




**KUHUSU** TARI MARATHON 2026
Katika kuadhimisha miaka 10 ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Taasisi imeandaa Marathon 2026 kama sehemu ya maadhimisho ya muongo mmoja wa mafanikio katika Utafiti,Usambazaji wa Teknolojia na Ushawishi wa Sera kwa Kilimo Endelevu.

Tukio hili linalenga kuunganisha jamii, wadau wa sekta ya kilimo na umma kwa ujumla katika kuhamasisha afya bora, lishe, na matumizi ya teknolojia za kisasa za kilimo kwa maendeleo endelevu ya Taifa.

**Malengo ya Marathon**
Kupitia marathon hii, Taasisi inalenga kuwawezesha wakulima wadogo ambao ni nguzo muhimu ya sekta ya kilimo nchini, kusaidia jamii zilizo katika mazingira magumu, na kuongeza uelewa kuhusu mchango wa tafiti za kisayansi katika kuendeleza kilimo chenye tija, endelevu na kinachoweza kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.




**Ushirikiano na Wadau**
Zaidi ya hayo, marathon hii inatoa jukwaa la kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi za utafiti, sekta binafsi na washirika wa maendeleo, ili kuhamasisha ubunifu, kubuni na kutekeleza suluhisho endelevu yatakayochochea maendeleo ya kilimo na kuleta manufaa ya kudumu kwa jamii.

**Aina za mbio**
Half Marathon (21 KM)- Kwa washiriki wenye uzoefu wa kati
10 KM Race-Mbio za ushindani na fitness
5KM Fun Run-Kwa jamii na washiriki wote

**Kauli Mbiu**
**UTAFITI KWA USALAMA WA CHAKULA-DIRA 2050**

**Faida za kushiriki TARI Marathon 2026**

Afya na Fitness
Inaboresha afya ya moyo, stamina na kupunguza magonjwa yasiyoambukiza.

**Afya**
Umoja wa Jamii
Inawaleta pamoja watu wa rika tofauti kujenga mshikamano wa kitaifa.

**Jamii**
Ukuaji wa Uchumi
Inaongeza biashara, utalii na fursa za ajira wakati wa tukio.

**Uchumi**
Mchango kwa wakulia wadogo wadogo
Kuchangia moja kwa moja katika kuunga mkono wakulima wadogo na jamii zilizo katika mazingira magumu.

**Wakulima**
Jiunge na TARI Marathon 2026
Usikose nafasi ya kuwa sehemu ya tukio kubwa la michezo, afya na maendeleo nchini Tanzania.

**Jisajili Sasa Jifunze Zaidi**
Limited slots available — jiandikishe mapema
Wadhamini na Washirika
TARI Marathon 2026 inafanikishwa na washirika mbalimbali kutoka sekta ya umma na binafsi wanaounga mkono afya, michezo na maendeleo ya jamii.


WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
TARI
HONGERA
Medrick Ndenga
Mfanyakazi Hodari
TARI Makao Makuu 2026.
TARI- Utafiti kwa Maendeleo ya Kilimo
Tufuatilie TARI Tanzania tari.tanzania TanzaniaTari TARI Tanzania


WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
TARI
HONGERA
Karoline Sichalwe
Mfanyakazi Hodari Kitengo
cha Utafiti na Ubunifu
2026.
TARI- Utafiti kwa Maendeleo ya Kilimo
Tufuatilie TARI Tanzania tari.tanzania TanzaniaTari TARI Tanzania


WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
TARI
HONGERA
Musa Mbogo
Mfanyakazi Hodari Kitengo
cha Uhaulishaji Teknolojia
na Mahusiano 2026.
TARI- Utafiti kwa Maendeleo ya Kilimo
Tufuatilie TARI Tanzania tari.tanzania TanzaniaTari TARI Tanzania


WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
TARI
HONGERA
Ezra Kamaninja
Mfanyakazi Hodari Kitengo
cha Tehama
2026.
TARI- Utafiti kwa Maendeleo ya Kilimo
Tufuatilie TARI Tanzania tari.tanzania TanzaniaTari TARI Tanzania


WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
TARI
HONGERA
Helladius Tumwesige
Mfanyakazi Hodari Kitengo
cha Ukaguzi wa ndani
2026.
TARI- Utafiti kwa Maendeleo ya Kilimo
Tufuatilie TARI Tanzania tari.tanzania TanzaniaTari TARI Tanzania


WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
TARI
HONGERA
Clara Lyimo
AFISA UGAVI II
MFANYAKAZI BORA 2026
TARI- Utafiti kwa Maendeleo ya Kilimo
Tufuatilie TARI Tanzania tari.tanzania TanzaniaTari TARI Tanzania


WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
TARI
HONGERA
Hamis Makungu
Mfanyakazi Hodari Kitengo
cha Mipango, Tathmini na Ufuatiliaji
2026.
TARI- Utafiti kwa Maendeleo ya Kilimo
Tufuatilie TARI Tanzania tari.tanzania TanzaniaTari TARI Tanzania


WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
TARI
HONGERA
Adv. Joachim Kamuli
(Afisa Sheria Daraja la pili)
Mfanyakazi Hodari Kitengo
cha Sheria 2026.
TARI- Utafiti kwa Maendeleo ya Kilimo
Tufuatilie TARI Tanzania tari.tanzania TanzaniaTari TARI Tanzania


WIZARA YA KILIMO
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA
TARI
HONGERA
Ebenezer Kisanga
Mfanyakazi Hodari Kitengo
cha Uhasibu na Fedha 2026.
TARI- Utafiti kwa Maendeleo ya Kilimo
Tufuatilie TARI Tanzania tari.tanzania TanzaniaTari TARI Tanzania

# MAJUKUMU YA UTAFITI KWA VITUO (RESEARCH MANDATES)







| Na. | KITUO | MAJUKUMU YA UTAFITI |
|---|---|---|
| 1. | TARI Uyole - Mbeya | Viazi mviringo, uhandisi kilimo, maharage, mahindi, pareto na mazao ya bustani |
| 2. | TARI Kifyulilo - Iringa | Viazi mviringo, maharage, mahindi, ngano na mazao ya bustani |
| 3. | TARI Ukiriguru - Mwanza | Pamba, mazao ya mizizi na mazao ya bustani |
| 4. | TARI Maruku - Kagera | Migomba, maharage na mazao ya bustani |
| 5. | TARI Selian - Arusha | Maharage, ngano na shayiri, mazao jamii ya mikunde na mazao ya bustani |
| 6. | TARI Tengeru - Arusha | Mazao ya bustani |
| 7. | TARI Naliendele - Mtwara | Mikorosho, karanga, ufuta na mazao ya bustani |
| 8. | TARI Ilonga - Morogoro | Mahindi ya Nyanda za chini, mazao jamii ya mikunde, alizeti, mtama, uwele, ulezi, teknolojia ya mazao baada ya mavuno na mazao ya bustani |
| 9. | TARI Dakawa - Morogoro | Mpunga na mazao ya bustani |
| 10. | TARI Ifakara - Morogoro | Mpunga na mazao ya bustani |
| 11. | TARI Tumbi - Tabora | Kilimo misitu (agroforestry) na mazao ya bustani |
| 12. | TARI Mlingano - Tanga | Udongo, mkonge na mazao ya bustani |
| 13. | TARI Kibaha - Pwani | Miwa na mazao ya bustani |
| 14. | TARI Mikocheni – Dar es Salaam | Nazi, bioteknolojia na mazao ya bustani |
| 15. | TARI Makutupora - Dodoma | Zabibu na mazao ya bustani |
| 16. | TARI Hombolo - Dodoma | Mazao himilivu kwa mabadiliko ya tabianchi: mtama, uwele, ulezi na mazao ya bustani |
| 17. | TARI Kihinga - Kigoma | Michikichi na mazao ya bustani |
| 18. | TARI TaCRI - Kilimanjaro | Kahawa na mazao ya bustani |
| 19. | TARI TORITA - Tabora | Tumbaku na mazao ya bustani |
| 20. | TARI TRIT - Iringa | Chai na mazao ya bustani |



**Mkurugenzi Mkuu**
**Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI)**
**S. L. P 1571, Dodoma**
**Tel: +255 26 2961 995/e-mail:dg@tari.go.tz**
**Website:www.tari.go.tz**

TariTanzania Tanzaniatari official_ taritanzania TARI Tanzania TARI

# VITUO VYA UHAULISHAJI TEKNOLOJIA




**TUFUATILIE**

TariTanzania · Tanzaniatari · official_taritanzania · TARI Tanzania · TARI